JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

## Jarida la Robo ya Kwanza ya Mwaka

## (Julai - Septemba)

Toleo Na. 0001 29, Septemba 2022



Chamwino_dc Chamwino Dc

# Waziri Bashe Akagua Miradi Mikubwa ya Kilimo, Chamwino




**Na Modesta Simon**

"Nimeridhishwa na mradi unavyoendelea, kazi iliyofanyika ni nzuri".

Maneno haya yamesemwa na Waziri wa Kilimo Mhe. Hussen Bashe alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya kilimo Wilayani Chamwino Septemba 28, 2022.

Miradi iliyokaguliwa ni mradi wa kilimo cha zabibu Chinangali na mradi wa ujenzi wa Bwawa la umwagiliaji Membe.

Katika miradi yote miwili Mhe. Bashe ameridhishwa na kazi inavyoendelea na ametoa maelekezo mbalimbali kwa wasimamizi wa miradi hiyo.

Kwenye mradi wa shamba la zabibu Chinangali wenye ekari 600, ameelekeza wakulima waliopo kwenye eneo lililobaki jirani na shamba hilo waorodheshwe na maeneo yao yaingie kwenye mradi huu ili wapate walau ekari 1000 kwa ajili ya kilimo cha mashamba makubwa( block farming).

Mhe. Waziri pia ameeleza adhima ya Serikali ya kujenga kiwanda cha kuchakata na kutengeneza mchuzi wa zabibu ambapo wakulima wataongeza thamani ya zao hilo nakuuza kwa bei nzuri kuliko wanavyouza sasa ikiwa ni pamoja na kuwa na soko la uhakika.

' Tukifanikiwa kujenga kiwanda maana yake wakulima watauza mchuzi wa zabibu. Kilo moja ya zabibu kwa sasa ni shilingi elfu moja lakini lita moja ya mchuzi wa zabibu ni shilingi elfu tatu, hivyo mkulima ataondokana na adha ya kukosa soko. Halmashauri pia itaweza kupata ushuru mzuri ( produce cess). Alisema Mhe. Waziri.

Naye Mwenyekiti wa chama cha ushirika cha CHABUMA AMCOS ndugu David Mwaka ameeleza kuwa kazi ya kusafisha shamba inaendelea vizuri, tayari wamesafisha kwa 99% na kazi ya kusambaza drippers inaendelea. Amemuomba Mhe. Waziri wazo lake la kujenga kiwanda alifanyie kazi kunusuru soko la zabibu.

" Mwaka huu zabibu nyingi zimeharibikia shambani tunakuomba lile wazo lako la kujenga kiwanda ulifanyie kazi kunusuru soko la zao la zabibu". Alisema Mwenyekiti wa CHABUMA AMCOS.

Akiwa kwenye mradi wa ujenzi wa bwawa Membe, Mhe. Waziri amempongeza Mkandarasi kwa kazi nzuri.

Vilevile Mhe. Bashe ametoa maagizo kwa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri kupitia upya na kuorodhesha wakulima wanaolima kwenye eneo la mradi wa Membe ili wapewe maeneo na eneo linalobaki litagawiwa kwa vijana.

"Naagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji mfanye upya mapitio ya wakulima wanaolima kwenye eneo la mradi ili tuwatambue na kuwagawia maeneo kama ni ekari 5 au 10 ili asije kuibuka mtu na kusema eneo lake limechukuliwa, na kisha eneo linalobaki tutaligawa 9kwa vijana. Tunataka kilimo chenye tija na kuondokana na ukulima mdogomdogo wa kujikimu". Alisema Mhe. Bashe.

Vilevile Mhe. Waziri ameelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kukaa na vyama vya ushirika na kufanya tathimini ya mavuno kwa wakulima wadogo waliokopeshwa fedha na benki ya CRDB ili kuona ni kiasi gani kinaweza kulipika na kwa wale ambao hawakuwa na mavuno mazuri waorodheshwe walipe kwa msimu ujao wa 2022/2023.

# Vijana wazalendo watembea kwa miguu wapita Chamwino




**Na Modesta Simon**

Vijana wazalendo( NEW AFRICAN YOUNG FIGHTERS) wanaotembea kwa miguu kutoka Dar es salaam kwenda Kagera kwenye kilele cha wiki ya vijana pamoja na tukio zima la kuzima Mwenge wa Uhuru litakalofanyika mkoani Kagera, leo tarehe 15 septemba, 2022 wamefika Ofisi ya Halmashauri ya Chamwino na kupokelewa na Afisa Utamaduni na Michezo ndugu Achimpota na kukutana na Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Dkt. Semistatus Mashimba.

Vijana hao wameeleza lengo la matembezi yao ni kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mpendwa mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayolifanyia Taifa letu, kama vile miundombinu katika Sekta ya Mawasiliano, Elimu , Afya, Umeme na mengine mengi mazuri.

Kauli mbiu matembezi yao ni " TUJITOKEZE KUCHANGIA DAMU ILI KUOKOA MAISHA YA MAMA ZETU WANAPOJIFUNGUA NA WANAOPATA AJALI", ALIPO MAMA NA VIJANA TUPO.

# Chamwino yazindua mkakati wa kuimarisha Ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya Elimu ya Msingi



Na Modesta Simon

Katibu Tawala wa Wilaya ya Chamwino Bi.Neema Nyarege amewataka Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kuwaandaa kikamilifu watahiniwa ili waweze kupata ufaulu wenye tija wa daraja A mpaka C na kuondoa ufaulu wa alama D na E kwa ngazi ya shule za msingi.

Bi.Nyarege ametoa tamko hilo wakati akizungumza na Viongozi wa Sekta ya Elimu ngazi ya Halmashauri pamoja na Waratibu Elimu Kata Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe.Gift Msuya kwenye uzinduzi wa kukabidhi Mkakati wa Kuimarisha Ujifunzaji na Ufundishaji katika ngazi ya Elimu Msingi tarehe 09.09.2022 wilayani Chamwino. Amesema kuwa shule za sekondari nazo zinatakiwa kuongeza ufaulu wa daraja la 1hadi 3 na kupunguza au kuondoa kabisa ufaulu wa daraja la 4 na daraja sifuri.

"Viongozi wa Elimu wasimamie nidhamu kwa wanafunzi na watumishi katika kuimarisha zoezi la ujifunzaji na ufundishaji katika taaisis zote aidha ushauri nasaha utolewe kwa wanafunzi ili waweze kukabiliana na changamoto watakazo kutana nazo katika ujifunzaji "amesema hayo Bi.Nyarege

Aidha Bi.Nyarege amesema kuwa wanafunzi watoro watambuliwe na warudishwe shuleni kupitia watendaji wa vijiji na Taarifa zitumwe katika ofisi ya Mkurugenzi kila ijumaa kabla au ifikapo saa 4 asubuhi ili ziweze kutumwa mkoani na wiki ya pili au inayofuata taarifa za idadi ya wanafunzi watoro waliorudi shuleni ziwasilishwe.

Bi Nyarege amesema "Ninafahamu kuwa Mwongozo ulizinduliwa rasmi tarehe 04.08.2022 mkoani Tabora na Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye pia alizungumzia Malengo ya Mwongozo wa uandikishaji wanafunzi darasa la kwanza ili kuhakikisha wanafunzi walioandikishwa wanamaliza elimu ya msingi kama walivyoanza.

Pia amesema kuwa Viongozi katika ngazi zote wahakikishe walimu wanatambuliwa, wanathaminiwa na kuwezeshwa pamoja na kushirikishwa, kutiwa moyo na kutobaguliwa.

Mbali na hayo amewataka walimu kuonyesha ushirikiano na kujitathmini huku akitaka Uteuzi wa Viongozi wa Elimu kuzingatia Weledi, Uzoefu na Ubunifu katika ngazi zote.

# Waheshimiwa Madiwani Chamwino Wapewa Elimu Kilimo cha Pamba



## Na Modesta Simon

Balozi wa zao la pamba nchini Agrey Mwanri ametoa elimu kuhusu kilimo cha zao hilo kwa Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chanwino.

Maelekezo hayo ameyatoa leo, Septemba 07, 2022 kwenye kikao maalum cha Baraza la Madiwani la mwaka kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri

Akizungumza kwenye kikao hicho Mwanri amesema Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imepangiwa kuvuna kilo milioni nne za pamba.

Aliendelea kueleza kuwa makubaliano yaliyowekwa ni walau kila Halmashauri izalishe mara mbili ya lengo walilopewa.

Mwanri alieleza kuwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wameelekezwa na Mhe. Rais kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Maelekezo ya namna ya kulima zao hilo la pamba kwa mavuno yenye tija yalitolewa ambapo kipimo ni sentimita 50 kwa 30 ambapo ukipanda kwa kipimo hiki unapata miche 4444 kwa ekari moja.

Balozi wa zao la pamba aliwahimiza wahe. Madiwani wawahimize wananchi kulima pamba kwani kupitia kilimo hicho Halmashauri itanufaika kwa kuongeza mapato pamoja na kukuza uchumi wa mwananchi mmojammoja na Halmashauri kwa ujumla.

Mkilima pamba Halmashauri itapata ushuru(produce cess) na hali ya maisha ya wananchi itakuwa nzuri." Alisema balozi wa pamba.

Aidha alieleza kuwa kwa wakulima watakaolima pamba wataletewa mbegu, viuatilifu na mifuko vitavyotolewa kwa mkopo na ambao utalipwa baada ya kuvuna na kuuza.

" Tutaleta mbegu, viuatilifu na mifuko vitakavyokopeshwa na mkulima ataulipa mkopo huo baada ya kuvuna na kuuza pamba yake." Alisema balozi wa pamba.

Alihimiza watumie fursa hiyo ambayo imetolewa na Serikali kwani kilimo cha pamba ulimaji wake hauhitaji mvua nyingi na kwa hali ya hewa ya Chamwino zao linaweza kustawi vizuri.

' Fursa hazitolewi, fursa zinachukuliwa, hivyo tumieni fursa hii iliyotolewa na Serikali kwani zao la pamba halihitaji mvua za kitimutimu kama zak la mpunga au miwa." Alisema balozi wa pamba.

Vilevile alitoa maelekezo ya mambo ya kuźingatia kwenye kupanda, kupalilia, kupuliza dawa, kuvuna pamoja na vifaa vinavyofaa kwa kuvunia kwa mavuno yenye tija. Pia alieleza kwa sasa bei ya pamba kwa kilo imepanda inauzwa kwa wastani wa shilingi 2200.

# Baraza la Madiwani Chamwino Latoa pongezi ukusanyaji wa Mapato



## Na Modesta Simon

Wajumbe wa Baraza la madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino wametoa pongezi kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Wahe. Madiwani, Mkurugenzi Mtendaji, Mweka Hazina na Menejimenti ya Halmashauri kwa kukusanya mapato ya ndani na kuvuka lengo kwa 126% na kuongoza kwa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

Pongezi hizo zimetolewa leo, Septemba 07, 2022 kwenye kikao Maalum cha Baraza la mwaka kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri.

Sambamba na pongezi hizo wajumbe wameshauri mambo mbalimbali yatakayosaidia Halmashauri kuendelea kufanya vizuri kwenye kukusanya mapato.

Kati ya mambo yaliyoshauriwa ni suala la watendaji wa vijiji kutoa ushirikiano kwenye ukusanyaji wa mapato. Ilishauriwa Mkurugenzi Mtendaji awape malengo ya kukusanya kwa kila kijiji.

Pia Kudhibiti utoroshaji wa mapato kwenye mageti, wakusanyaji mapato wa magetini wabadlishwe mara kwa mara, wasikae eneo moja kwa muda mrefu

Ilishauriwa pia kudhibiti utoroshaji wa mifugo minadani yajengwe maboma walau ya muda ya kwa ajili ya mifugo ambayo haijauzwa na ambayo imeuzwa kwa minada ambayo haina maboma hayo.

Vilevile ilishauriwafedha zilizokusanywa ziwasilishwe na kupelekwa benki mapema kuepuka fedha kutumika kinyume na utaratibu.




# Kamati ya Kudhibiti UKIMWi Chamwino yatoa Kadi za CHF Kwa Watoto

**Na Modesta Simon**

Wajumbe wa kamati ya kudhibiti UKIMWI wilaya ya Chamwino wakiongozwa na Mwenyekiti wa kamati hiyo Mhe. Keneth Yindi ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri wametembelea vituo vya tiba na mafunzo kwa wanaoishi na virus vya UKIMWI.

Shughuli hiyo imefanyika jumamosi Septemba 3, 2022 kwenye Kituo cha Afya Chamwino, Hospitali ya Mvumi Mission na Kituo cha Afya cha Mlowa Barabarani.

Wajumbe wameweza kuchangia na kutoa kadi za bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa ( CHF) kwa watoto wanaoishi na Vvu wapatao 230 kwa maeneo yote waliyoyatembelea.

Kituo cha Afya chamwino zimetolewa kadi kwa watoto 54, hospitali ya Mvumi Mission zimetolewa kadi kwa watoto 91 na kituo cha Afya cha Mlowa barabarani zimetolewa kadi kwa watoto 85.

Aidha watoto wamepewa mahusia mbalimbali ikiwemo suala la kusoma kwa bidii maana elimu ndio kitu cha pekee ambacho kinaweza kuweka usawa kwa wote katika jamii kati ya maskini na matajiri.

Akiongea na watoto hao Mchungaji Emmanuel Madeje ambaye pia ni mjumbe wa kamati alisema kilichowasukuma wao kama kamati kufanya jambo hilo ni upendo walionao kwa watoto hao. Akinukuu mistari ya Biblia alisema, " Mshike sana elimu, usimuache aende zake maana huyo ndiyo uzima wako."

" Silaha pekee itakayowasaidia katika maisha yao ni elimu. Elimu ndiyo itakayowapa heshima, hivyo ninyi mliopata fursa ya kuwa shuleni someni kwa bidii.^ Alisema Mchungaji.

Naye Mwenyekiti aliahidi kutoa zawadi ya vifaa vya shule kwa watoto watakaoshika nafasi ya kwanza hadi ya kumi kwa wanafunzi hao. Pia alisisitiza watoto kuweka bidii kwenye elimu, kjjituma na kujiamini na hapo ndipo watakapopata heshima kwenye jamii

Aliwataka pia kuzingatia masharti yote wanayoelekezwa na madaktari wao likiwemo suala la kufuatilia masuala ya unywaji wa dawa.

# Mwenge wa Uhuru Wapitisha Miradi yote Chamwino

**Na Modesta Simon**

Mwenge wa Uhuru Wilayani Chamwino umepitisha miradi yote sita iliyopangwa kutembelewa ambapo kati ya hiyo miradi mitatu ilizinduliwa, miradi miwili kuwekewa mawe ya msingi na kutembelea mabanda ya vikundi na kukabidhi hundi kwa kikundi cha vijana.

Katika mradi wa uzinduzi wa chanjo ya mifugo, uogeshaji na uvalishaji hereni kwa mifugo ilielezwa kuwa wanyama waliotambuliwa mpaka sasa ni ng'ombe 18,678, mbuzi 7,445, kondoo 2,797 na punda 237. Ambapo lengo la mradi ni kudhibiti magonjwa ya mifugo, utambuzi wa mifugo na kukuza kipato kwa wafugaji.

Aidha ilielezwa kuwa mradi utawezeaha kupunguza vifo vya mifugo na kuongezeka kwa mifugo, kuongezeka kwa kipato kwa wafugaji kutokana na kuongezeka kwa mifugo iliyo bora. Kurahisisha biashara ya mifugo na mazao yake wilayani, ndani na nje ya nchi. Kuwezesha wafugaji kupata mikopo na kuweka bima ya mikopo yao, kuongeza mapato ya Halmashauri na kutambulika kwa mifugo na umiliki wake.

Mradi mwingine uliotembelewa na mwenge



wa uhuru uwekaji wa jiwe la msingi kituo cha afya cha Itiso ambapo awamu ya kwanza utagharimu kiasi cha shilingi milioni 250 ambazo ni fedha kutoka Serikali kuu mfuko wa fedha za tozo kwa jengo la wagonjwa wa nje ( OPD), jengo la maabara na kichomea taka.

Mradi utawezesha kusogeza huduma bora za afya karibu na jamii na kuimarisha afya ya jamii.

Mradi wa maji Dabalo pia ulikuwa miongoni mwa miradi iliyozinduliwa na mwenge wa uhuru ambapo utakuwa na uwezo wa kuhudumia jumla ya wakazi 8134 wa kijiji cha dabalo. Mradi utawezesha upatikanaji wa maji safi na salama kwa jamii, kumtua mama ndoo kichwani, kupunguza muda wa kutafuta majiau kuyafuata mbali na badala yake kufanya shughuli nyingine za maendeleo na kiuchumi. Pia kuondoa magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na kukosekana kwa maji safi na salama na udhibiti wa mapato yanayotokana na mradi wa maji baada ya kufunga mfumo wa mita za malipo ya kabla.

Mradi umegharimu kiasi cha shilingi 1,127,470,348.01,kwa mchanganuo fedha kutoka Serikali Kuu shilingi 1,033,617,241.13, wahisani(MKAJI) shilingi 91,663,906.88 na jamii shilingi 2,189,200.00.

Mwenge wa Uhuru pia ulizindua madarasa ya UVIKO 19 ßhuale ya sekondari Msangaambayo yamegharimu kiasi cha shilingi 60,000,000/=

Mradi wa kikundi cha vijana wasakatonge unaojishughulisha na utoaji wa huduma za ufundi seremala kwa wakazi wa kijiji cha Buigiri na vijiji jirani ambacho kilipewa mkopo wa shilingi 15,000,000/= na halmashauri ili waweze kupanua na kuboresha biashara yao.Fedha ambayo inatokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya Halmashauri ambayo hutumika kuwezesha kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.0

Pia mwenge uliweka jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Mvumi km 1.1 ambao utagharimu shilingi 496,928,000/= . Mkandarasi tayari ameshalipwa shilingi 348,794,730.00 kiasi cha shilingi 148,133,270.00 kitalipwa kwa kazi ya umaliziaji na fedha za matazamio. Mradi utawezsaha kuwa na barabara za kudumu na zenye kupitika muda wote.

# Mkuu wa Wilaya Chamwino azindua kompyuta na printer kata ya Buigiri



**Na Modesta Simon**

Mkuu wa wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya amezindua matumizi ya kompyuta na printer, Agosti 17,2022 zilizonunuliwa kupitia kampeni ya NISHIKE MKONO KUINUA UBORA WA ELIMU CHAMWINO ambayo ilianzishwa na yeye mwenyewe.

Uzinduzi wa vifaa hivyo vya kompyuta umefanyika shule ya msingi buigiri ambapo mashine hizo zitagawiwa kwenye shule nne za msingi pamoja na ofisi ya Mratibu Elimu Kata kwa ajili ya kuchapa na kudurufu mitihani ambayo itasaidia katika kuwaandaa wanafunźi kufanya vizurk kwenye mitihani yao ya kitaifa na hivyo kuinua ubora wa elimu.

Akizungumza kwenye hafla hio amewapongeza na kuwashukuru wote waliochangia Kampeni hiyo ambapo kila kaya ilipaswa kuchangia kiasi cha shilingi elfu tano. Alisema jumla ya michango iliyopatikana ilikuwa ni shilingi milioni 107 na kata ya Buigiri iliweza kuchangia kiasi cha milioni 7.6

Aidha alieleza kuwa kupitia wadau waliweza,kukusanya kiasi cha shilingi milioni 28 ambazo ziligawanywa kwenye kata zilizofanya vizuri kwenye kukusanya michango ikiwemo kata ya buigiri.

Kata ya buigiri ilipatiwa shilingi milioni 4 ambazo zilipelekwa shule shikizi ya Mizengo pinda ambayo wananchi walijitolea hali na mali kujenga madarasa na Serikali kupita Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kupeleka milioni 60 kwa ajili ua kujenga madarasa 3 na ofisi ya walimu na hivyo wakaona wawaongezee nguvu kwa ajili ya kukamilisha ili shule iweze kuanza.

Milioni 10 ilipelekwa sekondari ya Ikowa ili kukarabati madarasa 3 na ofisi ya walimu na baadae waliongeza shilingi milioni 3 kwa ajili ya matundu ya vyoo baada ya kuona hakuna matundu ya vyoo.

Vilevile ilitolewa shilingi laki 4 kuwasaidia wanfunzi shule ya Nhinhi waliofaulu vizuri ili waende kidato cha tano na sita ambao wazazi walishindwa kuwapeleka shule kutokana na haoi duni ya maisha.

Mkuu wa wilaya alimshukuru Mhe Rais kwa kuwapelekea kiasi cha shilinngi bilioni 2,9 fedha za UVIKO 19 ambazo zilijenga vyumba vya madarasa164. Walishirikiana na jamii kufanya kazi ambazo hazikuwa na ulazima wa kutumia fedha pekee na kufanikiwa kuokoa fedha iliyosaidia kujenga ofisi 75 za walimu na kupata madawati kwa vyumba vyote.

Aidha akieleza kuwa wamefanikiwa kupata usajili wa shule shikizi 4 kati ya tisa walizoziombea usajili. Nyingine hazikufanikiwa kutokana na kukosa matundu ya vyoo, hivyo wamekubaliana na Mkurugenzi wa Halmashauri waweke kwenye bajeti hii iliyaweze kujengwa na shule zisajiliwe kli mwakani zianze kusajili wanafunzi.

Sambamba na kuzindua vifaa hivyo, Mkuu wa Wilaya pia amezindua mfumo ambao utatumika katika kuandaa mitihani ya kuwapima wanafunzi pamoja nakuona mahudhurio yao

Pia bendera nyekundu anbayo itapeperushwa kwa wazazi ambao hawatawapeleka watoto shuleni na ofisi ya kijiji ambayo itakuwa na kaya nyingi ambazo hazikupeleka watoto shuleni. Baada ya hàpo sheria zitachukuliwa dhidi ya wazazi hao.

Wakiongea kwa nyakati tofauti katika hafla hiyo. Mhe. Diwani wa kata ya buigiri na Mtendaji wa kata wamesema ili kuboresha elimu wanafunzi hawataruhusiwa kutoka nje ya kata mpaka kwa kibali kutoka uongozi wa kata ili kuwabaini ambao hawataripoti shueleni kwa wakati ili waweze kutafutwa na kurudishwa shuleni.

# Makarani wa Sensa Chamwino Wasisitizwa Kuhusu Umuhimu wa Sensa

**Na Modesta Simon**



Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amesisitiza juu ya umuhimu wa sensa kwa makarani wa Sensa, wasimamizi wa maudhui na wasimamizi wa TEHAMA.

Ameyasema hayo alipotembelea kituo cha mafunzo ya usimamizi wa sensa Wilayani Chamwino leo Agosti 17, 2022 ambacho kipo shule ya sekondari Chamwino.

" Haya mnayoyategemea kuyafanya kilà mtu ndio anayaangalia. Mwisho wa mwaka mtu atakuwa anaomba takwimu. Naomba takwimu za mifugo ili nipange mipango, naomba niapte takwimu za wilaya za uchumi za uchumi wa wananchi wangu ili nipange mipango." Alisema mkuu wa mkoa.

Vilevile amesisitiza matumizi ya lugha kuwa lugha itakayotumika na makarani wa sensa iwe ni lugha fasaha na sahihi ya watanzania ambayo ni kiswahili. Hategemei watumie lugha ambayo wale wanàowauliza hawaielewi.pia amewataka watumie lugha yenye staha, lugha ambayo inaweza kueleweka lakini inatunza heshima ya unayeongea nae..

"Mtumie lugha yenye staha, lugha ambayo inaweza kueleweka lakini inatunza heshima ya yule ambaye unaongea naye. Lugha yenye staha ni lugha ambayoinamuonyesha mtu kuwa wewe ni rafiki yake, wewe ni ndugu yake, wewe ni Mtanzania mwenzake, lugha ambayo inamuondolea hofu ya kutokukuamini, lugha ambayo akikusikiliza atajenga imani kuwa ni mtu sahihi kwa sababu ni mtu anayeaminika." Alisema Mkuu wa mkoa.

Pia alizungumza kuhusu kujenga mahusiano mazuri na wale unaokwenda kuwahoji maswali, alitolea mafano unaingia kwenye kaya hujasalimia wenye nyumba unaanza moja kwa moja kuwahoji maswali. Kwa kufanya hivyo huwezi kupata taarifa za sensa kwani tayari utakuwa umempotezea shauku au hamu ya kukujibu.

"Sisi watanzania tunajua jinsi salamu ilivyo na umuhimu kwa utamaduni wetu." Alisema mkuu wa mkoa.

Aidha mkuu wa mkoa amesisitiza kuhusu suala la mavazi kuwa muonekano wa mavazi unaweza kumthibitishia unayemuhoji kuwa unaaminika na hivyo akajenga imani ya kukupa taarifa.

Alitilia mkazo suala la muda nakueleza kuwa waangalie mazingira wanayokwenda kufanyia zoezi la sensa, lakini kuwapangia muda watakaokwenda kuwahoji na kujipanga wao wenyewe. Ili kama ni nyumba ambayo huwa habaki mtu basi siku hiyo mtu awepo kwa ajili ya kutoa taarifa.

Aidha aliwataka watu wa TEHAMA kuitumia vizuri na kueleza kuwa TEHAMA imekuwa na mchango mkubwa sana kwa maendeleo lakini ikitumika vibaya imekuwa na madhara makubwa.

" Niendelee kusisitiza tumieni vizuri TEHAMA, ukikosea tu tarakimu moja mtu kakwambia anahekari 3 wewe ukaandika 33 hebu ona jinsi ambavyo umebadlilisha taarifa za matokeo ya tunachokitarajia na ambavyo utakwenda kuathiri mipango mnataka kuifanya. Kuweni makini na wale ambao wanajua hawako makini, zoezi hili wasilifanye. Maana hapo ndipo panakwenda kumalizia kazi nzuri ya kukusanya taarifa na kufanya mpate taarifa sahihi.' Alisema mkuu wa mkoa.

Makarani pia wametahadharishwa kumiepusha na ulevi mpaka watakapokuwa wamekabidhi kazi. Pia viongozi wengine wa kamati ya ulinzi na usalama walitoa tahadhari kwa mtu atakaye haribu zoezi la sensa kuwa atakuwa amefanya hujuma na hjvyo atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alitoa rai kwa wananchi wa mkoa wa dodoma kutoa taarifa sahihi bila hofu kwa makarani wa sensa kwa sababu wamewezeshwa na ana imani watafanya kazi nzuri kwani Serikari imejiridhisha nao. Aliomba wawaamini na wawape taarifa sahihi na zote ambazo zinatakiwa kutolewa.

Pia aliomba wannchi watoe taarifa pale ambapo watapata kikwazo kwenye zoezi la sensa. Na ili kutekeleza hilo alizindua namba maalum itakayotumika kupiga pindi inapotokea changamoto ambayo ni 0800110083.

# Chamwino Yang'ara Chanjo ya UVIKO 19





UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
DODOMA REGIONAL COMMISSIONER'S OFFICE

Certificate of Achievement

This certificate is awarded to

Chamwino District Council

*in recognition of the 1st Performance in Covid-19 Vaccination by 10th August, 2022*

*Hon. Rosemary S. Senyamule*
*Regional Commissioner*
DODOMA

*Dr. Fatuma R. Mganga*
*Regional Administrative Secretary*
DODOMA

**Na Modesta Simon**

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetunukiwa vyeti viwili maalum kwa kuongoza na kuwa ya kwanza kitaifa kwa 90% ya uchanjaji wa chanjo ya UVIKO 19 na imeongoza kwa halmashauri za mkoa wa Dodoma kwa kuwa na matokeo yasiyoshuka katika utoaji wa chanjo hiyo.

Vyeti hivyo vimekabidhiwa na Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule kwenye kikao cha tathimini ya utekekezaji wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022 na taarifa ya utekelezaji wa kampeni harakishi ya utoaji wa chanjo ya UVIKO 19.

Kikao kilifanyika ukumbi wa mikutano wa mkuu wa mkoa wa Dodoma Alhamisi wiki hii.

Mkuu wa mkoa ameipongeza Halmashauri kwa kufanya vizuri kwenye zoezi hilo la utoaji wa chanjo ya UVIKO 19.)

# Naibu Waziri Muungano na Mazingira Afanya Ukaguzi Shughuli za uchimbaji Madini, Nayu, Chamwino

**Na Modesta Simon**



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis amefanya ziara ya kukagua shughuli za uchimbaji wa madini katika eneo la msitu wa hifadhi wa Chinyami kijiji cha Nayu kata ya Dabalo Wilayani Chamwino.

Ziara hiyo imefanyika leo Agosti 10,2022 ambapo alikutana na kufanya mazungumzo na wawekezaji ( wachimbaji wadogo) pamoja na wananchi wa eneo hilo.

Katika ziara hiyo Naibu waziri amebaini baadhi ya taratibu za uchimbaji kukiukwa na hivyo ametoa maelekezo kwa wachimbaji hao wayatekeleze ndani ya mwezi mmoja na ikiwa watashindwa kufanya hivyo watafungiwa kuendelea na shughuli hizo za uchimbaji.

Mhe. Naibu waziri ameelekeza wachimbaji hao waende Taasis zote zinazohusika na utoaji wa vibali vya uchimbaji madini ikiwemo Wakara wa misitu(TFS), Bonde la maji Wami - Ruvu na NEMC waombe vibali.

"Nendeni kwenye taasis zote zinazohusika mkapate vibali. Tunataka uwekezaji wenye tija utakaokuwa na faida kwa wote." Amesema Naibu Waziri.

Vilevile Naibu Waziri ametoa mwezi mmoja kwa wachimbaji kutengeneza utaratibu mzuri wa kudhibiti maji yanayotumika kuosha dhahabu yasilete athari kwa binadamu na mazingira.

" Maji yenye sumu yanaweza kuleta magonjwa kama mapafu na miti inaweza isiote. Athari ya sumu huipati leo.Maji hayo yanatiririka na kwenda kwenye vyanzo vya maji na watu wanayatumia kulima, kufuga samaki, kunywa, kuoga." Amesema Naibu Waziri.

Rai pia imetolewa kwa wote wanaotorosha madini na ameomba waache mara moja na badala yake madini yanayopatikana kwenye eneo hilo yauzwe kwenye masoko ya madini ili kuiwezesha Serikali kupata mapato.wanaotorosha madini watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Serikali yetu inahitaji mapato. Kuna watu wanatorosha madini. Kuna masoko ya kuuzia madini. Jambo hilo liachwe, kauze madini sehemu halali inayohusika. Ukitorosha sheria itakuandama." Amesema Naibu Waziri.

# Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino yapata Cheti cha Ushindi




Halmashauri ya Wilaya ya chamwino imepata cheti cha ushindi kwa kuwa mshindi wa tatu katika kundi la Halmashauri za mkoa wa Dodoma kwenye sherehe za sikukuu ya wakulima - Nanenae 2022 zilizofanyika kwenye viwanja vya nanenane, Nzuguni Dodoma.

Cheti hicho kilikabidhiwa kwenye hafla ya kufunga maonesho ya nanenane kanda ya Kati kwa Mikoa ya Dodoma na Singida.

## Mkuu wa Mkoa Ashauri Kujengwa kwa Hosteli Viwanja vya Nanenane Nzuguni

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,Rosemary Senyamule ameongeza muda wa siku mbili wa maonyesho ya wakulima 88 hadi Agosti10Mwaka huu ili kuongeza tija ya kilimo4 katika suala zima la kutoa Elimu kwa wakulima na Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ameshauri kujengwa kwa Hosteli za wakulima katika Viwanja vya nanenane vilivyopo Nzuguni mkoani Dodoma ili wakulima wawe wanapata muda wakupata Elimu kuhusu kanuni za kilimo bora wakati ambapo maonyesho yatakuwa yameisha ili Kila Mwezi wakulima Kila Halmashauri waende kujifunza.

Hata hivyo ametoa Wito kwa Kila Halmashauri kupelekea idadi ya wakulima kufika katika maonyesho ya nanenane kupata maarifa na kujifunza masuala mapya yaliyopo katika sekta ya kilimo.

Kwa Upande wake Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba amesema kuwa uzalishaji wa mazao agenda ya 10/30 mkoa umejipanga kuzalisha tani 600,000za Alizeti ili kuondokana na uhaba wa mafuta ya kula na kuongeza tija ya mazao.

Aidha Serukamba ameomba Maonyesho ya nanenane Kanda ya Kati yawe kwenye ramani ya Dunia ili kupanua wigo katika Nchi mbalimbali kushiriki ili Kampuni kubwa zenye teknolojia kutoa fursa ya kutoa Elimu kwa wananchi.

# Chamwino Yang'ara UMISSETA Mkoa, 2022




**Na Modesta Simon**

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imefanya vizuri kwenye mashindano ya michezo kwa shule za Sekondari (UMISSETA) mkoa wa Dodoma yaliyoshirikisha Halmashauri 8 za mkoa wa Dodoma.

Katika mashindano hayo Halmashauri ya wilaya ya Chamwino imefanikiwa kuchukua makombe 6, kwa nafasi ya kwanza na ya pili.

Makombe yaliyopatikana kwa kushika nafasi ya kwanza ni kwa michezo ya volleyball wavulana na wasichana, netball, kwaya, ngoma na sanaa.

Kwa ushindi wa nafasi ya pili makombe yalipatikana kwa michezo ya basketball na mpira wa miguu kwa wasichana.

Aidha katika mashindano hayo Halmashauri imefanikiwa kutoa wanafunzi 33 waliochaguliwa kwenye timu ya mkoa na walimu watatu wa michezo ya volleyball, netball na kwaya.

Pongezi zimetolewa kwa wote waliofakisha ushindi huu kupatikana.

# Chamwino Yaweka Mikakati Kuinua ufaulu Darasa la Saba



**Na Modesta Simon**

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeweka mikakati ya kuinua ufaulu kwenye mtihani wa darasa la saba. Mikakati hiyo imewekwa kwenye kikao kazi kilichofanywa na watumishi wa Idara ya Elimu Msingi ngazi ya Halmashauri, Maafisa Elimu Kata na walimu Wakuu.

Kikao hicho kimefanyika leo, Jula 27, 2022 kwenye shule ya msingi Buigiri Blind iliyopo kata ya Buigiri.

Katika kikao hicho mikakati mbalimbali ya kuondoa daraja D na E kwenye matokeo ya mtihani wa Taifa wa darasa la saba imewekwa na walimu wamekubaliana kuisimamia kwa nguvu zote.

Vilevile walimu wameweka mikakati ya kuhakikisha ufaulu wa daraja A unaongezeka kwa kiwango kikubwa ili kuiwezesha Wilaya kufanya vizuri na hivyo kushika nafasi nzuri kwenye matokeo ya Mtihani wa Taifa wa darasa la saba.

Kikao kiliongozwa na Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Bibi Zaina Kishegwe.

# Uwekaji wa Jiwe la Msingi Mradi wa Maji, Dabalo Wlayani Chamwino




**Na Modesta Simon**

Waziri wa Maji Aweka Jiwe la Msingi Mradi wa Maji DabaloMheshimiwa Jumaa Aweso Waziri wa maji ameweka jiwe la msingi kwenye mradi wa maji Kata ya Dabalo wilayani Chamwino,leo Julai 15, 2022. Mradi huu umetekelezwa kwa kutumia teknojia mpya ya matenki kutoka PLASCO na umegharimu zaidi ya shilingi milioni 900.Uwekaji huo wa jiwe la msingi ulihudhuriwa pia na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Utumishi Mhe. Deogratius Ndejembi ambaye mradi huo upo katika Jimbo lake la Chamwino.Ilielezwa kuwa Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu Hassan yupo kazini kumtua mama Ndoo kichwani.

# Chamwino Yatoa Mkulima Bora Nanenane Kanda ya Kati



**Na Modesta Simon**

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imefanikiwa kutoa mkulima bora kanda ya kati kwa mikoa ya Dodoma na Singida. Hayo yalibainishwa kwenye maadhimisho ya sikukuu ya wakulima (nanenane) kanda ya kati yaliyofanyika viwanja vya nanenane Nzuguni mkoani Dodoma.

Mkulima huyo anayejulikana kwa majina ya Aliseni Cosmasi Damian kutoka kijiji cha Magungu aliweza kulima hekari mia moja za zao la alizeti na mtama. Mkulima huyu aliongoza kwa kupata jumla ya alama 95%

Alipoulizwa kitu kilichomsukuma kuwekeza katika suala la kilimo Bwana Aliseni alieleza kuwa alisikia kwenye vyombo vya habari kuwa kuna uhitaji mkubwa wa mafuta ya kula nchini, na hivyo akaamua kutumia fursa hiyo.

“ Nilisikia kupitia vyombo vya habari vikitangaza kuhusu uhaba mkubwa wa mafuta ya kula, ndipo nikaona ipo haja yakutumia fursa hiyo.” Alisema.

Vilevile alieleza kuwa kuhusu suala la Mtaji alisikia kupitia vyombo vya habari kuwa Halmashauri ya Chamwino inatoa mikopo kwa wakulima ikishirikiana na benki ya CRDB, kwa wakulima waliojiunga na AMCO’s hivyo na yeye alipeleka mahitaji yake na alifanikiwa kuwezeshwa.

Aidha Bwana Aliseni ameishukuru sana Halmashauri ya Wilaya ya Chàmwino pamoja na benki ya CRDB kwa uwezeshaji huo na aliwashauri wakulima wengine wanaposikia fursa kama hizi wasisite kuzitumia kwani ndio njia ya kujiletea maendeleo.

Bwana Aliseni amesema anatarajia kupata wastani wa magunia 12 kwa ekari na hivyo kuwa na uwezo wa kulipa mkopo wa CRDB na kubaki na mapato kwa ajili ya kujikimu na shughuli nyingine za maendeleo.

“ Matarajio yangu ni kupata gunia 12 kwa kila hekari baada ya mavuno ambapo nitaweza kurejesha mkopo wa CRDB na nitabaki pia na fedha kwa ajili ya kujikimu pamoja na shughuli za maendeleo.” Alisema.

# Waziri Bashe Azindua Usajili wa Wakulima na Mwongozo wa Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea




## Na Modesta Simon

Mheshimiwa waziri wa Kilimo Hussen Bashe amefanya uzinduzi wa usajili wa wakulima na mwongozo wa utoaji wa ruzuku ya mbolea msimu wa 2022/2023 ambao utafanyika kidigitali.

Uzinduzi huo ameufanya leo Julai 4, 2022 kwenye ukumbi wa Serikali ya kijiji cha Chamwino Wilayani Chamwino. Katika uzinduzi huo Mhe Bashe aliongozana na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. David Silinde. Viongozi wengine waliohudhuria ni Katibu Mkuu na Naibu katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Wakuu wa Wilaya wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Kisarawemameneja wa VODACOM na Benki ya CRDB na Mkurugenzi mtendaji toka TFRA.

Katika uzinduzi huo Mhe. Waziri ameeleza kuwa Serikali imeshanunua mashine za kupima udongo143 ambazo zitagawiwa kwenye Halmashauri zitakazotumika kupima afya ya udongo kwenye mashamba ya wakulima na baada kupima mkulima atashauriwa eneo lake linapaswa kulima mazao gani au atumie virutubisho gani au mbolea itakayoendana na eneo lake. Na akishapimiwa atapewa cheti kitakachoonyesha matokeo ya kipimo.Aidha ameeleza kuwa huduma hio itatolewa bure.

Vilevile Mhe. Waziri ameeleza kuwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan anaumizwa na umasikini wa watu wa Tanzania. Kokote anakozungumza utasikia akizungumzia kuboresha kilimo na kuondoa umasikini. Na Mhe. Rais hajaishia tu kusema, ukichukua bajeti ya kilimo ya mwaka huu wa fedha ni zaidi ya shilingi tilioni moja na haijakwenda kwenye posho wala vikao.

Mhe. Waziri pia ameeleza kuwa kwenye sherehe za nanenane mwaka huu Mhe. Rais Mama Samia Suluhu Hassan atashuhudia utiaji saini wa mikataba ya umwagiliaji yenye thamani ya bilioni 400 ambazozitakwenda kujenga skimu za umwagiliaji.

Vilevile Mhe. Waziri ameeleza kuwa Serikali imetenga kiasi cha shilingi ilioni 150 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Katika mapinduzi ya kilimo Wizara imepanga imepanga kufanya kilimo cha mfano cha mashamba makubwa (block farming) kwa mkoa wa Dodoma katika Wilaya ya Chamwino na Bahi ambapo jumla ya zaidi ya hekta elfu 23, na kwa Chamwino pekee zimetengwa hekta elfu 20 na mashamba haya yanakwenda kuajiri vijana, na wataanza na kilimo cha alizeti na watapewa umiliki wa miaka 30 adi 60 juu ya umiliki wa hati kuu. Na kwa block tatu za Chamwino moja ya kata ya Membe yenye hekta 8000 itakuwa ya skimu ya umwagiliaji.Katika uzinduzi huo Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Gift Isaya Msuya alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka.

HALMASHAURI YA WILAYA

CHAMWINO

Chamwino Buigiri

Chamwino Dc

Chamwino_dc

www.chamwinodc.go.tz

S.L.P 1126 Dodoma